

# Chanjo ya RTS,S yaonyesha ni salama na ina uwezo wa kupunguza maambukizi ya malaria kwa watoto wadogo wilayani Korogwe

## Taasisi zinazohusika

Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Kituo cha Tanga, Tanzania  
Taasisi ya Afya na Magonjwa ya Ukanda wa Joto (LSHTM), Uingereza,  
CMP, Chuo Kikuu Copenhagen, Denmark  
PATH Malaria Vaccine Initiative, Marekani  
GlaxoSmithKline, Ubeljiji



## Utangulizi

Ugonjwa wa malaria ni tatizo kubwa katika jamii yetu na hasa maeneo ya tambarare. Unaathiri watu wote lakini zaidi ni watoto chini ya miaka mitano. Zipo njia mbalimbali za kujikinga na malaria ambazo tunazifahamu. Kama tujuavyo, katika mapambano inabidi kutumia mbinu mbalimbali kwani tunajitahidi kutafuta chanjo ya malaria ili iweze kusaaidiana na mbinu zilizopo kama vile vyandarua, dawa ya kupulizia mbu, na dawa za kutibu malaria. RTS,S ni chanjo mpya ya malaria iliyo mstari wa mbele kabisa katika majaribio. RTS,S ni chanjo inayoandaa kinga ya mwili kukabiliana na vimelea vya malaria vya *Plasmodium falciparum* punde vinapoingia kwenye mfumo wa damu na kuanza kushambulia chembe hai za ini. Kinga hii huzuia vimelea kuendelea kukua na kuzaliana kwenye ini na hatimaye tena kushambulia mfumo wa damu ambapo mtu akipata maabukizi haya huanza huonyesha dalili za ugonjwa. Ili kutengeneza kinga hii dhidi ya vimelea vya malaria, chanjo ya RTS,S imeunganisha kipande muhimu cha protini ijulikanayo kitaalam kama circumsporozoite (CS) (kipande hiki cha protini husaidia vimelea vya malaria kuwa na uwezo wa kupenya na kuingia kwenye ini) kwenye kipande cha protini kinachopatikana kwenye chanjo ya homa ya ini ya GSK Biologicals. Kwa kutumia mfumo maalum wa kuandaa chanjo wa GSK unauwezesha mwili kutengeneza kinga bora zaidi.

## Utaratibu

Utafiti ulifanyika Korogwe, Tanzania, na Kilifi, Kenya, katika kipindi cha 2007 na 2008 ukihusisha watoto 894 wenye umri wa miezi 5-17 na ulifanyika kwenye utaratibu wa kutoa chanjo kwa watoto wadogo (EPI). Utafiti wa Korogwe ulihusisha watoto 447 kutoka vijiji 18 na ulifanyika kwenye zahanati za Ngombezi, Makuyuni na Mbaghai. Dr. Lorenz von Seidlein na Dr. John Lusingu wa NIMR waliongoza huu utafiti. Lengo kuu lilikuwa kuthibitisha kuwa chanjo ya malaria ya RTS,S inaweza kuzuia ugonjwa wa malaria na ni salama kwa kutumia mfumo wa kuandaa chanjo wa GSK ujulikanayo kama ASO1. Watoto walioshiriki kwenye utafiti huu waligawanywa kwenye makundi mawili yaliyo sawa kwa idadi, kundi moja lilipata chanjo ya RTS,S katika mizunguko mitatu; kundi la pili lilikuwa linganishi lilochanjwa dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa (rabies).

## Matokeo

Chanjo ya malaria ya RTS,S/ASO1 ilionyesha kupunguza kuugua malaria kwa asilimia 53 baada ya kufanya ufuatiliaji uliodumu kwa wastani wa miezi 8 kwa pande zote mbili (Korogwe na Kilifi). Dr. Lusingu amesema kuwa matokeo haya yamethibitisha kuwa hii chanjo ya malaria iliweza kupunguza kwa kiasi kikubwa watoto wadogo kuugua malaria. Dr. Martha Lemnge wa Taasisi ya NIMR kituo cha Tanga anasema “Huu ni wakati wa kufurahia katika historia ya utafiti na mbinu za kupambana na malaria kwani chanjo yenye ubora ya malaria inaongeza uwezo wa kupambana na malaria kwa kushirikiana na mbinu zingine kama vile vyandarua vyenye viatilifu” Akitoa maoni juu ya matokeo haya, Mkurugenzi Mkuu wa NIMR Dr. Andrew Kitua amesema taasisi yake “imefurahishwa na hatua zilifikwa mpaka sasa na anatarajia kushirikiana na washirika wengine ili hatimaye kutokomezwa malaria”. Taarifa ya utafiti huu ilichapishwa kwenye jarida la kimataifa la sayansi litwalo New England Journal of Medicine kule Marekani la tarehe 11 Desemba, 2008. Aidha hapa nchini taarifa ya hii chanjo ilitolewa kwa wadau wa sekta ya Afya na nyingine kule Dar mwezi Januari, 2009.

## Hitimisho

Tathmini kubwa ya awamu ya tatu itaanza 2009 na itahusisha watoto 16,000 katika vituo 11 vya nchi saba za Afrika ikiwemo Tanzania. “Tumejipanga vyema kushiriki kwenye tathmini kubwa ya awamu ya tatu itakayohusisha vituo vingi” anahitimisha Dr. Lusingu.

## Shukrani

Tunatoa shukrani kwa watoto na wazazi/walezi wote walioshiriki katika utafiti, Tunashukuru wafadhili wetu (PATH MVI, GSK Bio na INDEPTH-Malaria Clinical Trials Alliance). Shukrani za dharti ni kwa: Uongozi wa ngazi zote Wilaya ya Korogwe, Zahanati zote zilizohusika, Hospitali ya Wilaya ya Korogwe (Magunga), Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) Makao Makuu na Wafanyakazi wote wa mradi wa RTS,S.

Kwa Taarifa zaidi wasiliana na: Dk Martha Lemnge, Mkurugenzi, NIMR Tanga, Tanga (+255 27 26 46084, mobile +255 784 929 611); Email : [mlemnge@tanga.mimcom.net](mailto:mlemnge@tanga.mimcom.net)

Au Dk John Lusingu, Mkuu wa Mradi wa RTS,S Korogwe (+255 787 679 515); Email: [jlusingu@tanga.mimcom.net](mailto:jlusingu@tanga.mimcom.net)